**Maswali na Majibu**

*1.* Mungu aliambia Musa afanye nini Waisraeli waliponun'gunika kwamba hakuna maji?
*Aliambia Musa azungumze na mwamba kule Kadeshi*

2. Musa alifanya nini? *Alipiga mwamba mara mbili.*

*3.* Mungu aliadhibu Musa namna gani kwa kutomtii kikamilifu?
*Musa hakukubaliwa kuenda kwa Nchi ya Ahadi.*

*4.* Mungu alikuwa anatufundisha somo gani juu ya Yesu?
*Yesu ana nguvu kama mwamba. Alipigwa (sulibiwa) ili atupe uhai.*

*5.* Musa aliharibu hilo somo namna gani?
*Alipiga mwamba mara mbili. Yesu alisulibiwa mara moja tu.*

6. Musa atakubaliwa kuingia kwa Nchi ya Ahadi? Kama ndiyo, lini?
*Ndiyo. Yesu atakapokuja atamfufua Musa kutoka kwa wafu*.

7. Mbona Mungu alituma nyoka za moto kwa kambi?
*Kuwaadhibu Waisraeli kwa kunun'gunika*.

*8.* Nani aliwaombea Waisraeli? *Musa.*

9. Waisraeli wangepona namna gani wakiumwa na nyoka?
*Kama wangeangalia nyoka ya shaba yenye Mungu aliambia Musa atengeneze*.

*10.* Nyoka ya shaba inatufundisha somo gani juu ya Yesu?
*Yesu aliinuliwa juu kwa msalaba. Tukimwamini tutaokolewa.*

## Mistari ya kukariri

Yohana 3:14 – 16 Yohana 6:48 – 50

## Mazungumzo

Mungu alitumia vitu fulani kwa Agano la Kale kutufundisha masomo juu ya vile Yesu atakuja kuokoa watu kutoka dhambini. Zungumza juu ya somo tunalo soma kutoka kwa: 1) musa akipiga mwamba
2) Nyoka ya shaba kwa mti

## Kuandika

Jifanye kwamba wewe ni Mwisraeli jangwani. Andika vile ungejisikia wakati maisha yalikuwa magumu, hakuna maji ni mana tu ya kukula. Eleza ni nini ilifanyika kwa familia yako nyoka za moto zilipokuja kwa kambia.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 15 Safari ya jangwani – 2

**SOMA Hesabu 20:1 – 13; Hesabu 21:4 – 9; Yohana 3:14 – 16**

**SOMO**

Mungu alisema kwamba Waisraeli watatangatanga jangwani kwa miaka arobaini kwa sababu hawakumwamini. Musa aliwaongoza Waisraeli kutoka kwa mpaka wa Nchi ya Ahadi na kurudi nyuma kwa jangwa.

Waisraeli hawakupenda kuishi jangwani. Waliishi kwa mahema na kulikuwa kumekauka na vumbi nyingi. Walifika Kadeshi kwa jangwa la Sini. Hawakupata maji ya kunywa na walikuwa na kiu sana. Waisraeli hawakukumbuka vile Mungu alikuwa amewapa maji wakati mwingine kule jangwani. Hawakuamini Kwa Mungu na wamuombe.

Badala yake walienda kwa Musa na kulalamika. Walisema, "Mbona ulitutoa Misri na kutuleta huku pahali penye maisha ni magumu. Tulikuwa na chakula cha kutosha kule Misri lakini hapa, tutakufa kwa ajili ya kiu." Musa alienda mlangoni mwa Maskani akainamisha uso wake na kuomba Mungu. Utukufu wa Mungu ulionekana kwake na Mungu akamwambia, nena na mwamba wa Kadeshi na maji yatoke halafu watu watakunywa.

Mapema walipokuwa kwa hii safari yao kule Horebu, Waisraeli walinun'gunika kwa sababu hakukuwa na maji. Wakati huo Mungu aliambia Musa achukue fimbo yake na **apige** mwamba uliokuwa Herobu na maji yalitoka na Waisraeli walikunywa. Lakini wakati huu pale Kadeshi, Mungu aliambia Musa achukue fimbo mkononо na a**ambie** mwamba na Mungu atafanya maji yatoke ili watu wakunywe.

Mosea alikasirikia watu. Alichukua fimbo yake na akapaza sauti, "Sikiliza enye waasi, ni lazima tumtolee maji kwa huu mwamba?" Halafu akapiga mwamba mara mbili. Maji yalitoka na watu wakanywa. Lakini Mungu hakufuraia Musa. Ni Mungu aliyeleta maji kutoka kwa mwamba wala si Musa au Haruni. Musa alikasirika na hakutii kikamilifu vile Mungu alikuwa amesema. Mungu alimwambia Musa anene na mwamba lakini Musa alipiga mwamba mara mbili.

Kama adhabu kwa kutotii Mungu kwa imani, Musa hakukubaliwa kuingia kwa Nchi ya Ahadi. Hii ilikuwa adhabu kali sana. Musa alikuwa amewaongoza Waisraeli jangwani kwa miaka 40 na sasa hataingia kwa hiyo nchi.

Hii inatufundisha kwamba ni vyema kutii Mungu kamili. Katika Agano la Kale, Mungu alituonyesha kukuja kwa Yesu kwa njia mbalimbali. Hapa Mungu anatufundisha juu ya Yesu lakini Musa akaharibu kwa kupiga mwamba tena. Musa alikuwa amepiga mwamba kule Horebu kuwawezesha watu wakunywe maji. Mara ya pili Mungu alitaka Musa anene na mwamba. Lakini Musa alipiga mwamba mara mbili.

| **Maji kutoka kwa mwamba** | **Yesu** |
| --- | --- |
| Mwamba ni wa **nguvu** na **haubadiliki** | Yesu ako kama mwamba. Uwezo wa Yesu ni wa **Nguvu.** Upendo wake kwetu **haubadiliki** |
| Maji yanatuweka hai. Bila maji tutakufa. Musa alipiga mwamba ku-wapa watu maji wakunywe ili wasikufe. | Yesu mwamba wetu,alisulibiwa ili tuwe na tumaini la uzima wa milele. |

Mungu alikuwa anafunza somo alipoambia Musa kutoa maji kutoka kwa mwamba. Yesu alikuwa afe mara moja tu. Musa aliharibu somo alipopiga mwamba mara mbili.

Baada ya muda mrefu, mwisho wa miaka 40, Mungu aliambia Musa apande mlima mrefu uliokuwa karibu na nchi ya Kanaani. Kutoka kwa huo mlima Musa aliweza kuona Nchi ya Ahadi. Lakini hakuweza kwenda huko. Yesu atakaporudi kuwa Mfalme, atamfufua kutoka kwa wafu. Pale ndiyo Musa ataishi kwa Ufalme wa Mungu milele.

Waisraeli waliendelea na kusafiri jangwani. Mara tu walianza kunun'gunika tena. Walisema kwamba walikuwa wamechoka na safari iliyokuwa ngumu muno. Waliambia Musa , "Mbona ulitutoa Misri na tukufie huku jangwani? Hakuna chakula! Hakuna maji! Hatutaki hiki chakula kisicho kitamu!" Hawa watu walikuwa wakinun'gunikia Mungu. Aliwapa mana ya kukula. Aliwapa maji ya kukunywa. Lakini bado walinun'gunika.

Mungu aliwakasirikia Waisraeli. Hawakumshukuru kwa aliyowafanyia. Walinun'gunika tu. Mungu alituma nyoka za moto kwenye kambi yao. Punde tu nyoka za moto zilitokea. Waisraeli walikimbia kwa mahema hali wakilia kwa hofu. Lakini nyoka zilijinyonganyonga mpaka hemani. Nyoka ziliwauma. Nyoka zilikuwa za sumu na watu wengi walikufa. Wengi walilala kwa mahema wagonjwa sana kwa kuumwa na nyoka. Walikuwa na maumivu sana kwa ajili ya kuumwa kwa nyoka. Kila mtu alikuwa na uoga.


Waisraeli walimwendea Musa. Walisema, "Tumekosa. Tulikosa kunun'gunika.Tafadhali tuombee kwa Mungu, muulize atusamehe na atuondolee hawa nyoka." Kwa hivyo Musa aliwaombea.

Mungu alimwambia Musa atengeneze mfano wa nyoka kutoka kwa shaba halafu aweke juu kwa mti. Mungu alisema kwamba yeyote atakayeumwa kwa nyoka ya moto na angalie nyoka ya shaba, atapona.

Musa alitengeneza nyoka ya shaba, na akaiweka juu kwa mti. Akawambia kwamba mtu yeyote atakayeumwa na nyoka lazima angalie nyoka ya shaba aliye juu kwa mti. Mkiangalia nyoka ya shaba juu, mtapona. Waisraeli wengi waliokuwa wameumwa na nyoka waliamini kwamba Mungu atawaponya. Walipoangalia yule nyoka wa shaba walipona.

Mungu alikuwa anatufundisha sisi somo kwa yule nyoka ya shaba. Alikuwa anatufundisha somo juu ya Yesu. Nyoka ya shaba aliinuliwa juu kwa mti. Kila mtu aliyeamini na aiangalie hakukufa. Walipona na wakaishi. Yesu aliinuliwa msalabani. Mtu yeyote akiamini kwa Yesu na kutii Mungu hata kufa milele. Atakuwa na uzima wa milele.

**Nyoka ya shaba**



*iliinuliwa kwa mti*
*Watu walitakiwa kuamini*
*na kutii Mungu*
*Halafu walipona na*
*waliokowa uzima wao*

**Jesu**



*aliinuliwa juu msalabani*
*Lazima tuamini kwa Yesu*
*na kutii Mungu*
*Tutaokolewa na tuwe*
*na uzima wa milele*